



TANZANIA INSURANCE REGULATORY AUTHORITY

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA

**GUIDELINES TO THE INSURANCE INDUSTRY ON THE
ACTUARIAL FUNCTION**

**MIONGOZO KWA SEKTA YA BIMA KUHUSU
KITENGO CHA TAKWIMU BIMA**

Revised Version No. 1.0

Toleo Liliboreshwa Na. 1.0

DECEMBER, 2024

DESEMBA, 2024

TABLE OF CONTENTS	YALIYOMO
SECTION ONE: INTRODUCTION	SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI
1.1 Authorization and Powers.....1	1.1 Idhini na Mamlaka.....1
1.2 Citation.....1	1.2 Nukuu.....1
1.3 Background and Rationale.....1	1.3 Usuli na Mantiki.....1
1.4 Application and Scope.....1	1.4 Matumizi na Mawanda.....1
1.5 Purpose and Objective.....2	1.5 Lengo na Madhumuni.....2
1.6 Interpretation and Acronyms.....3	1.6 Tafsiri na Vifupisho vya Maneno.....3
SECTION TWO: GENERAL PRINCIPLES	SEHEMU YA PILI: KANUNI ZA JUMLA
2.1 General Principles.....5	2.1 Kanuni za Jumla.....5
SECTION THREE: ACTUARIAL FUNCTION	SEHEMU YA TATU: KITENGO CHA TATHMINI BIMA
3.1 Qualification of Head of Actuarial Function.....6	3.1 Sifa ya Mkuu wa Kitengo cha Tathmini Bima.....6
3.2 Roles of Actuarial Function.....7	3.2 Majukumu ya Kitengo cha Tathmini Bima.....7
SECTION FOUR: APPOINTED ACTUARY	SEHEMU YA NNE: MTATHMINI BIMA ALIYETEULIWA
4.1 Qualification of Appointed Actuary.....11	4.1 Sifa za Mtathmini bima aliyeteuliwa.....11

TABLE OF CONTENTS	YALIYOMO
SECTION FIVE: SPECIFIC REQUIREMENTS	SEHEMU YA TANO: MAHITAJI MAALUM
5.1 Financial Condition Report.....15	5.1 Taarifa ya Hali ya Fedha.....15
5.2 Actuarial Valuation Report.....15	5.2 Taarifa ya Utathmini wa Bima.....15
SECTION SIX: REPORTING REQUIREMENTS	SEHEMU YA SITA: MAHITAJI YA TAARIFA
6.1 Reporting for Actuarial Function.....16	6.1 Utoaji wa Taarifa kwa Kitengo cha Utathmini Bima..16
6.2 Reporting for Appointed Actuary.....17	6.2 Utoaji wa Taarifa kwa Mtathmini aliyeteuliwa.....17
SECTION SEVEN: ENFORCEMENT	SEHEMU YA SABA: UTEKELEZAJI
7.1 Enforcement.....19	7.1 Utekelezaji.....19
SECTION EIGHT: REVIEW AND APPROVAL	SEHEMU YA NANE: MAPITIO NA IDHINI
8.1 Review of the Guidelines.....20	8.1 Mapitio ya Miongozo.....20
8.2 Effective Date.....20	8.2 Tarehe Rasmi ya Kuanza Kutumika.....20
8.3 Approval of the Guidelines.....20	8.3 Idhini ya Miongozo.....20

SECTION ONE: INTRODUCTION		SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI	
1.1 Authorization and Powers	These Guidelines are issued under Section 6 (2) (e) and 11 (b) of the Insurance Act Cap 394 which mandates the Authority to formulate and enforce standards in the conduct of the business of insurance which shall be observed by insurance registrants.	1.1 Idhini na Mamlaka	Miongozo hii imetolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (2) (e) na 11 (b) cha Sheria ya Bima Sura Ya. 394 ambacho kinaiwezesha Mamlaka kuweka vigezo vya uendeshaji wa shughuli za bima ambavyo vitatakiwa kuzingatiwa na watoa huduma za bima.
1.2 Citation	These Guidelines may be cited as “ <i>Guidelines to the Insurance Industry on the Actuarial Function</i> ”	1.2 Nukuu	Miongozo hii inafahamika kama “ <i>Miongozo Kwa Sekta Ya Bima Kuhusu Kitengo Cha Tathmini Bima</i> ”
1.3 Rationale	The rationale of these guidelines is to guarantee that an insurer possesses a adequate actuarial function capable of assessing and offering guidance to the insurer on, at least, estimation of liabilities, adequacy of premium, pricing of products, product design and adherence to relevant statutory and regulatory obligations.	1.3 Mantiki	Mantiki ya miongozo hii ni kuhakikisha kwamba kampuni ya bima ina kitengo cha tathmini bima chenye ujuzi wa kutosha kinachoweza kufanya uchambuzi na kutoa mwongozo kwa kampuni ya bima juu ya angalau, makadirio ya madeni, utoshelevu wa ada za bima, mchakato wa kupanga bei za bidhaa za bima, ubunifu wa bidhaa za bima na kufuata wajibu wa kisheria na usimamizi.
1.4 Application and Scope	These Guidelines are applicable to appointed actuarial firms, actuaries and all insurers registered in the United Republic of Tanzania. Unless otherwise stated, the term “insurer” in	1.4 Matumizi na Mawanda	Miongozo hii itatumika na kampuni za tathmini bima zilizoteuliwa, mtathmini bima aliyeteuliwa pamoja na kampuni zote za bima zilizosajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SECTION ONE: INTRODUCTION		SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI	
	these Guidelines includes both an insurer and reinsurer.		Isipokuwa imeelezwa vinginevyo, neno “kampuni ya bima” katika miongozo hii inajumuisha kampuni ya bima na kampuni ya bima mtawanyo.
1.5 Purpose and Objectives	<p>These Guidelines intend to;</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Establish a mechanism of regulating and supervising activities of Appointed actuarial firms, appointed actuaries and actuarial functions of Insurers; ii. Provide duties of Appointed actuarial firms, appointed actuaries and roles of the actuarial functions of insurers; iii. Reinforce the professional standards expected of an appointed actuarial firms, appointed actuary and actuarial units of insurers in carrying out specified duties and overall responsibilities as a control function; and iv. Provide guidance for the operation of the Actuarial functions established by Insurers. 	1.5 Lengo na Madhumuni	<p>Miongozo hii inakusudia;</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Kuanzisha utaratibu wa kusimamia shughuli za kampuni za tathmini bima zilizoteuliwa, watathimini bima walioteuliwa na kitengo cha tathmini bima cha kampuni ya bima; ii. Kuainisha majukumu ya kampuni za tathmini bima zilizoteuliwa, wataalamu wa tathmini bima walioteuliwa, na nafasi za kitengo cha tathmini bima cha makampuni ya bima; iii. Kuimarisha viwango vya kitaalamu vinavyotarajiwa kutoka kwa mtathmini bima aleyeteuliwa katika kutekeleza majukumu yake maalumu na wajibu wake kwa ujumla kama kazi ya udhibiti; na iv. Kutoa mwongozo wa uendeshaji wa kazi za kitengo cha tathmini bima kilianzishwa na kampuni ya bima.

SECTION ONE: INTRODUCTION		SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI	
<p>1.2 Interpretation and Acronyms</p>	<p>Act: means the Insurance Act Cap 394</p> <p>Authority: means Tanzania Insurance Regulatory Authority established under the Insurance Act.</p> <p>Commissioner: means the Commissioner of Insurance appointed under Section 7(1) of the Act</p> <p>Appointed Actuary: means an external and independent actuarial firm and actuary with qualifications specified in these guidelines.</p> <p>Actuarial Function: is a department/unit/section of a company that consists of one or more associate actuaries and actuarial candidates to assist and support the actuarial work of the company as required in these guidelines.</p> <p>Insurer: means an insurer as defined under section 3 of the Act.</p> <p>Financial Condition Report (FCR): means a written report to assess the financial condition of an Insurer.</p> <p>Actuarial Valuation Report: means a document for conveying Appointed Actuary's professional conclusion and recommendations to ensure that</p>	<p>1.6 Tafsiri ya maneno vifupisho vya maneno</p>	<p>Sheria: Maana yake ni Sheria ya Bima Sura ya 394</p> <p>Mamlaka: maana yake ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Bima.</p> <p>Kamishna: maana yake ni Kamishna wa Bima aliyeteuliwa chini ya Kifungu cha 7(1) cha Sheria.</p> <p>Mtathmini bima aliyeteuliwa: inamaanisha mtathmini bima wa nje na aliye huru mwenye sifa zilizoainishwa katika miongozo hii.</p> <p>Kitengo cha tathmini Bima: ni idara / kitengo / sehemu ya kampuni ambayo ina mtathmini bima mmoja au Zaidi mwenye sifa zilizoainishwa kwenye miongozo hii.</p> <p>Bima: maana yake ni bima kama ilivyoelezwa chini ya Kifungu cha 3 cha Sheria.</p> <p>Taarifa ya Hali ya Kifedha (FCR): inamaanisha taarifa iliyoandaliwa kwa ajili ya kutathmini hali ya kifedha ya kampuni ya bima.</p> <p>Taarifa ya Utathmini Bima: inamaanisha taarifa ya kuwasilisha mjumuisho na mapendekezo ya</p>

SECTION ONE: INTRODUCTION		SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI	
	<p>insurer is aware of the significance of the Appointed Actuary's opinion and findings.</p> <p>Board means Insurer's Board of Directors.</p>		<p>mtathimi bima aliyeteuliwa kuhahakisha kwamba kampuni ya bima inatambua umuhimu wa maoni na matokeo ya kazi yake.</p> <p>Bodi inamaanisha Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Bima.</p>

SECTION TWO: INSURERS ACTUARIAL SERVICE REQUIREMENTS		SEHEMU YA PILI: MAHITAJI YA HUDUMA ZA KITATHMINI BIMA KWA MAKAMPUNI YA BIMA	
2.1 Requirements	<p>2.1.1 An insurer shall be required to set up a robust actuarial function that is well positioned, resourced and staffed for proper operation.</p> <p>2.1.2 The insurer shall be required to engage an appointed actuary subject to approval by the Authority.</p> <p>2.1.3 The actuarial function and the appointed actuary shall be required to have access to and periodically report to the Board.</p>	2.1 Mahitaji	<p>2.1.1 Kampuni ya Bima itahitajika kuanzisha kitengo cha utathmini bima thabiti ambacho kina rasilimali za kutosha kwa ajili ya utendaji madhubuti.</p> <p>2.1.2 Kampuni ya Bima itamteua mtathmini bima kulingana na idhini ya Mamlaka.</p> <p>2.1.3 Kitengo cha tahmini bima na mtathmini bima aliyeteuliwa watapaswa kuwa na uwezo wa kufikia na kuwasilisha taarifa kwa Bodi kwa kipindi husika.</p>

SECTION THREE: QUALIFICATION, ROLES AND FUNCTION OF HEAD OF ACTUARIAL UNIT		SEHEMU YA TATU: SIFA, MAJUKUMU NA KAZI ZA MKUU WA KITENGO CHA TATHMINI BIMA	
3.1 Qualification of Head of Actuarial Function	<p>3.1.1 The Head of Actuarial Function shall:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Have a minimum of bachelor's degree in actuarial studies, statistics and mathematics or relevant qualifications and with 3 years post-qualification work experience; ii. Has enrolled in the recognized and reputable actuarial professional bodies or institutions within or outside Tanzania; and iii. Be a citizen of Tanzania. 	3.1 Sifa ya Mkuu wa Kitengo cha Tathmini Bima	<p>3.1.1 Mkuu wa Kitengo cha Tathimini Bima atapaswa:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Kuwa na angalau na shahada ya tathmini bima katika masomo ya utathimini bima pamoja na uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitatu (3) baada ya kuhitimu; ii. Awe amesajiliwa na taasisi au vyama vya wataalamu wa tathmini bima vinavyotambulika na vyenye hadhi, ndani au nje ya Tanzania; na iii. Kuwa raia wa Tanzania.
3.2 Roles of Actuarial Functions	<p>3.2.1 The actuarial function shall be required to have access to and periodically report to the Board on matters such as:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Circumstances that may have a material effect on the insurer from an actuarial perspective; 	3.2 Majukumu ya kitengo cha Tathmini Bima	<p>3.2.1 Kitengo cha tathmini bima kinapaswa kuwa na ufikiaji kwa kipindi husika kwa Bodi juu ya masuala kama:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Hali ambazo zinaweza kuathiri kampuni ya bima kwa mtazamo wa kitathmini bima; ii. Makadirio na dhana za madeni;

SECTION THREE: QUALIFICATION, ROLES AND FUNCTION OF HEAD OF ACTUARIAL UNIT		SEHEMU YA TATU: SIFA, MAJUKUMU NA KAZI ZA MKUU WA KITENGO CHA TATHMINI BIMA	
	<ul style="list-style-type: none"> ii. Estimates and assumptions for liabilities; iii. Prospective solvency position and cash flow of the insurer; iv. Adequacy of Actuarial Models used in providing output for preparation and presentation of financial statements; and v. Any other matters as determined by the Board. <p>3.2.2 The actuarial function shall be required to evaluate and provide advice on the following:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Risks facing insurer; ii. Insurer's investment policies and valuation of assets; iii. Insurer's current and prospective solvency position, including a calculation of capital requirements and liabilities for regulatory purposes. iv. Risk assessment and management policies and controls relevant to 		<ul style="list-style-type: none"> iii. Uwezo wa kulipa madeni ya kibima ya baadae mtiririko wa fedha wa kampuni ya bima; iv. Utoshelevu wa miundo ya utathmini bima inayotumika kutoa matokeo ya kuandaa na kuwasilisha taarifa za kifedha; Na v. Mambo mengine yoyote yatakayotajwa na Bodi. <p>3.2.2 Kitengo cha tathmini Bima kinapaswa kutathmini na kutoa ushauri juu ya yafuatayo:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Hatari zinazokabili kampuni ya bima; ii. Sera za uwekezaji wa kampuni ya bima na tathmini za mali; iii. Hali ya sasa na ya baadae ya ukwasi ikiwa ni pamoja na hesabu ya mahitaji ya mtaji na madeni kwa madhumuni ya usimamizi. iv. Tathmini ya vihatarishi na sera za uongozi na udhibiti unaofaa kwa

SECTION THREE: QUALIFICATION, ROLES AND FUNCTION OF HEAD OF ACTUARIAL UNIT		SEHEMU YA TATU: SIFA, MAJUKUMU NA KAZI ZA MKUU WA KITENGO CHA TATHMINI BIMA	
	<p>actuarial matters or financial condition of the insurer;</p> <p>v. Distribution of surplus;</p> <p>vi. Underwriting policies;</p> <p>vii. Reinsurance arrangements;</p> <p>viii. Product development and design, including the terms and conditions of insurance contracts;</p> <p>ix. Scenario and sensitivity testing;</p> <p>x. Sufficiency and quality of data used in the calculation of liabilities; and</p> <p>xi. Risk modelling and use of internal models, where applicable.</p>		<p>masuala ya tathmini bima au hali ya kifedha ya kampuni ya bima;</p> <p>v. Ugawanyaji wa kiasi cha ziada;</p> <p>vi. Sera za uandikishaji bima;</p> <p>vii. Mikataba ya bima mtawanyo;</p> <p>viii. Utengenezaji na uundaji wa bidhaa za bima kwa kuzingatia vigezo na masharti ya mikataba ya bima;</p> <p>ix. Upimaji wa mabadiliko ya hali;</p> <p>x. Utoshelevu na ubora wa data zilizotumika katika hesabu ya madeni; Na</p> <p>xi. Muundo wa vihatarishi na matumizi ya miundo ya ndani, ikiwa inafaa.</p>
3.3 Access to information	3.3.1 The actuarial function must have access to the insurer's Board, External Auditors and Internal Auditors as required.	3.3 Upatikanaji wa Taarifa	3.3.1 Kitengo cha tathmini bima kinapaswa kuwa na mawasiliano na Bodi ya kampuni ya bima, Wakaguzi wa Nje na Wakaguzi wa Ndani kama inavyotakiwa.
3.4 Role of Insurer	3.4.1 An insurer must ensure that the actuarial function has access to all relevant data, information, reports and staff of the insurer, and must take all reasonable steps to	3.4 Majukumu ya Kampuni ya Bima	3.4.1 Kampuni ya Bima inapaswa kuhakikisha kitengo cha tathmini bima kina ufikiaji wa taarifa ghafi, taarifa, ripoti na rasilimali watu wa kampuni ya bima, na kuchukua

SECTION THREE: QUALIFICATION, ROLES AND FUNCTION OF HEAD OF ACTUARIAL UNIT		SEHEMU YA TATU: SIFA, MAJUKUMU NA KAZI ZA MKUU WA KITENGO CHA TATHMINI BIMA	
	ensure access to all relevant service providers of the insurer, that its actuarial function reasonably believes are necessary to fulfill its responsibilities.		hatua zinazofaa ili kuhakikisha ufikiaji wa watoa huduma za bima kwa kampuni ya bima husika, ambazo kitengo cha tathmini bima kinaamini ni muhimu katika kufanikisha majukumu yake.

SECTION FOUR: QUALIFICATION, ROLES AND FUNCTION OF THE APPOINTED ACTUARY		SEHEMU YA NNE: MTATHMINI BIMA ALIYETEULIWA	
4.1 Qualification of appointed actuary	<p>4.1.1 The Appointed Actuary shall:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Be an actuarial firm that locally registered and licensed by the Authority; ii. Has minimum capabilities to perform valuations of actuarial liabilities for an insurer and debt evaluation, capital management, stress and scenario testing, investment and financial statements analysis; iii. Has ability to prepare and analyse IFRS 17 Reports; 	4.1 Sifa za Mtathmini bima aliyeteuliwa	<p>4.1.1 Mtathmini Bima aliyeteuliwa anatakiwa:</p> <ul style="list-style-type: none"> i) Kuwa kampuni ya tathmini bima iliyosajiliwa na Mamlaka nchini; ii) Kuwa na uzoefu katika kufanya tathmini ya kihesabu kwa kampuni za bima na awe anashiriki kikamilifu katika kutoa ushauri kwa kampuni za bima kuhusu tathmini ya madeni, usimamizi wa mitaji, na utoaji wa taarifa za kifedha. iii) Kuwa na uwezo wa kuandaa na kufanya uchambuzi wa IFRS 17; iv) Awe amsajiliwa na kupewa leseni na Mamlaka;
4.2 Appointment, Approval and Duration	<p>4.2.1 An insurer shall appoint an Actuary with prior approval of "Commissioner" for each financial year not later than one month before end of the relevant year.</p> <p>4.2.2 The responsibility for nominating the appointed actuary lies with the Board. In carrying out this responsibility, the Board must ensure that the appointment is in</p>	4.2	<p>4.2.1 Kampuni ya Bima inapaswa kuteua Mtathmini bima kwa idhini ya "Kamishna" kwa kila mwaka wa fedha si zaidi ya mwezi mmoja kabla kuisha kwa mwaka husika.</p> <p>4.2.2 Wajibu wa kumteua Mtathmini bima ni wa Bodi. Wakati wa kutekeleza jukumu hilo, Bodi inalazimika kuhakikisha kuwa uteuzi</p>

SECTION FOUR: QUALIFICATION, ROLES AND FUNCTION OF THE APPOINTED ACTUARY		SEHEMU YA NNE: MTATHMINI BIMA ALIYETEULIWA	
	<p>accordance with the requirements set out in these Guidelines.</p> <p>4.2.3 An appointed actuary shall be appointed for a fixed term of four (4) years, with an option to extend for an additional four (4) years, not exceeding a total of eight (8) years. After the completion of this period, a different appointed actuary must be appointed to ensure independence and objectivity. An appointed actuary who has been rotated off the audit of an insurer may resume the role as an appointed actuary after a lapse of four (4) years from the last engagement with that insurer.</p>		<p>huo unazingatia mahitaji yaliyowekwa katika Miongozo hii.</p> <p>4.2.3 Mtathmini Bima aliyeteuliwa atateuliwa kwa kipindi cha miaka minne (4), na chaguo la kuongeza kwa miaka mingine minne (4), pasipo kuzidi jumla ya miaka sita (6). Baada ya kumalizika kwa kipindi hiki, mkaguzi tofauti lazima ateuilwe ili kuhakikisha uhuru na uwazi. Mtathmini Bima aliyeteuliwa ambaye amesitishwa kwenye ukaguzi wa kampuni ya bima anaweza kurudi kuteuliwa kama Mtathmini Bima aliyeteuliwa baada ya kupita kwa miaka minne (4) tangu uteuzi wa mwisho na kampuni hiyo ya bima.</p>
4.3 Removal of appointed actuary	<p>4.3.1 If an Appointed Actuary resigns or is replaced, the insurer shall notify the Authority and give the reasons for the resignation or replacement. Such a notification shall include a statement of whether or not there were any</p>	4.3 Mabadiliko ya Mtathmini Bima aliyeteuliwa	<p>4.3.1 Ikiwa Mtathmini bima aliyeteuliwa atajiuzulu au kubadilishwa, kampuni ya bima itapaswa kutoa taarifa kwa Mamlaka na kutoa sababu za kujiuzulu au kubadilisha. Taarifa hiyo itaainisha ikiwa ilikosekana na makubaliano na Mtathmini</p>

SECTION FOUR: QUALIFICATION, ROLES AND FUNCTION OF THE APPOINTED ACTUARY		SEHEMU YA NNE: MTATHMINI BIMA ALIYETEULIWA	
	<p>disagreements with the former Appointed Actuary over the content of the actuary's opinion on matters of risk management, required disclosures, scopes, procedures, or data quality, and whether or not such disagreements were resolved to the former Appointed Actuary's satisfaction.</p> <p>4.3.2 The Authority may require an insurer to replace an Appointed Actuary when such person fails to adequately perform required functions or duties, is subject to conflicts of interest or no longer meets eligibility requirements.</p>		<p>bima wa zamani juu ya maudhui ya maoni ya masuala ya usimamizi wa vihatarishi, ufichuzi unaohitajika, mawanda, taratibu, au ubora wa taarifa, na ikiwa kutokubaliana huko kulitatuliwa kwa kuridhika kwa Mtathmini bima wa zamani aliyochaguliwa.</p> <p>4.3.2 Mamlaka inaweza kuitaka kampuni ya bima kubadilisha Mtathmini bima aliyeteuliwa iwapo atashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo, mgongano wa kimaslahi au kutokidhi matakwa yanayostahili.</p>

SECTION FIVE: FINANCIAL CONDITION REPORT AND ACTUARIAL VALUATION REPORT		SEHEMU YA TANO: TAARIFA YA HALI YA FEDHA NA TAARIFA YA TATHMINI WA BIMA	
5.1 Financial Condition Report	<p>5.1.1 The insurer shall produce a Financial Condition Report (FCR) duly prepared by the Appointed Actuary for each financial year.</p> <p>5.1.2 The FCR shall include items under Appendix 1.</p>	5.1 Taarifa ya Hali ya Fedha	<p>5.1.1 Kampuni ya Bima itaandaa Taarifa ya Hali ya Fedha (FCR) iliyoandaliwa Mtathmini bima aliyeteuliwa kwa kila mwaka wa fedha.</p> <p>5.1.2 Taarifa ya Hali ya Fedha (FCR) itajumuisha mahitaji yaliyoainishwa kwenye Kiambatisho 1.</p>
5.2 Actuarial Valuation Report	<p>5.2.1 The insurer shall produce Actuarial Valuation Report (AVR) duly prepared by appointed actuary as per provision of the Act.</p> <p>5.2.2 The Actuarial Valuation Report shall include items under Appendix 2.</p>	5.2 Taarifa ya Utathmini wa Bima	<p>5.2.1 Kampuni ya Bima itatengeneza Taarifa ya Utathmini wa Bima (AVR) iliyoandaliwa na Mtathmini bima aliyeteuliwa kulingana na kifungu cha Sheria.</p> <p>5.2.2 Taarifa ya Utathmini (AVR) itajumuisha mahitaji yaliyoainishwa kwenye Kiambatisho 1.</p>



SECTION SIX: REPORTING REQUIREMENTS		SEHEMU YA SITA: MAHITAJI YA TAARIFA	
6.1 Reporting for Actuarial Function	<p>6.1.1 The head of actuarial function shall report to the Board:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Any matter that may have an adverse material impact on the insurer's solvency or financial condition; ii. Any circumstance that may have a material effect on the insurer from an actuarial perspective; iii. Adequacy of the assumptions and estimates of insurance contract liabilities and other liabilities; iv. The adequacy of reinsurance contract held assets; v. If the insurer is in contravention of, or the actuarial function considers that the insurer is likely to contravene, any provisions of the Act, Regulations or any requirements concerning capital 	6.1 Utoaji wa Taafifa kwa Kitengo cha Tathmini Bima	<p>6.1.1 Kiongozi wa kitengo cha tathmini kitawasilisha taarifa ifuatayo kwa Bodi:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Suala lolote ambalo linaweza kuwa na athari mbaya kwenye ukwasi wa kampuni ya bima au hali ya kifedha; ii. Hali yoyote ambayo inaweza kuwa na athari kwa kampuni ya bima kwa mtazamo wa utathmini bima; iii. Utoshelevu wa dhana na makadirio ya madeni ya mkataba wa bima na madeni mengine; iv. Utoshelevu wa mali za mikataba ya bima mtawanyo; v. Ikiwa kampuni ya bima inaenda kinyume, au imekiuka kitengo cha utathmini bima na kinazingatia kwamba kampuni ya bima imekiuka kifungu chochote cha Sheria, Kanuni zake au matakwa yoyote yanayohusu utoshelevu wa mtaji, ukwasi na hali ya kifedha.

SECTION SIX: REPORTING REQUIREMENTS		SEHEMU YA SITA: MAHITAJI YA TAARIFA	
	<p>adequacy, solvency or financial condition;</p> <p>6.1.2 The head of actuarial function must report to the Authority directly and immediately in circumstances where the insurer has:</p> <ol style="list-style-type: none"> i. breached or is likely to breach solvency requirements; ii. ceased holding effective reinsurance contract held assets; <p>6.1.3 The head of actuarial function shall is required to report to the Authority directly and immediately where an insurer or its directors may have contravened the Act, or any other law and the contravention may prejudice the interests of the policyholders.</p>		<p>6.1.2 Mtathmini bima aliyeteuliwa ni lazima awasilishe kwa Mamlaka moja kwa moja hali ambayo inaashiria kwamba kampuni ya bima:</p> <ol style="list-style-type: none"> i. imekiuka au inaelekea kukiuka matakwa ya ukwasi; ii. haina mali za mikataba ya bima mtawanyo madhubuti; <p>6.1.3 Mtathmini bima aliyeteuliwa aliyeteuliwa anatakiwa kuwasilisha taarifa moja kwa moja kwa Mamlaka iwapo kampuni ya bima au wakurugenzi wake wamekiuka Sheria ya bima au Sheria nyingine na ukiukwaji huo unapoteza maslahi ya wakata bima.</p>
6.2 Reporting for Appointed Actuary	<p>6.2.1 The Appointed Actuary of an insurer shall submit to the Board a Quarterly Solvency Statement determined in accordance with the Regulations and generally accepted actuarial principles.</p> <p>6.2.2 The insurer shall submit to the Authority:</p>	6.2 Utoaji wa Taarifa Mtathmini Aliyeteuliwa	<p>6.2.1 Mtathmini bima aliteuliwa atapaswa kuwasilisha kwenye Bodi taarifa ya Ukwasi ya robo mwaka kwa mujibu wa Kanuni za bima na Kanuni za tathmini bima.</p>

SECTION SIX: REPORTING REQUIREMENTS		SEHEMU YA SITA: MAHITAJI YA TAARIFA	
	<ul style="list-style-type: none"> i. A Financial Condition Report duly prepared by the Appointed Actuary within four months of the end of each financial year; ii. Annual Solvency Statement determined in accordance with the Regulations and generally accepted actuarial principles at the end of each year; <p>6.2.3 The Appointed Actuary must report to the Authority directly and immediately in circumstances where the insurer has</p> <ul style="list-style-type: none"> i. breached or is likely to breach solvency requirements; ii. ceased holding effective reinsurance contract held assets; <p>6.2.4 The Appointed Actuary is required to report to the Authority directly and immediately where an insurer or its directors may have contravened the Act, or any other law and the contravention</p>		<p>6.2.2 Kampuni ya bima itawasilisha kwa Mamlaka:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Taarifa ya Hali ya Fedha iliyoandaliwa na Mtathmini bima aliyeteuliwa ndani ya miezi minne baada ya kuisha kwa mwaka wa fedha husika; ii. Taarifa ya Ukwasi ya kila mwaka itaandaliwa kwa mujibu wa Kanuni za bima na Kanuni za tathmini bima kila baada ya mwaka kuisha; <p>6.2.3 Mtathmini bima aliyeteuliwa ni lazima awasilishe kwa Mamlaka moja kwa moja hali ambayo inaashiria kwamba kampuni ya bima:</p> <ul style="list-style-type: none"> iii. imekiuka au inaelekea kukiuka matakwa ya ukwasi; iv. haina mali za mikataba ya bima mtawanyo madhubuti; <p>6.2.4 Mtathmini bima aliyeteuliwa aliyeteuliwa anatakiwa kuwasilisha taarifa moja kwa moja kwa Mamlaka iwapo kampuni ya</p>

SECTION SIX: REPORTING REQUIREMENTS		SEHEMU YA SITA: MAHITAJI YA TAARIFA	
	<p>may prejudice the interests of the policyholders.</p> <p>6.2.5 Where such a report is made directly to Authority, the Appointed Actuary is not under any obligation to disclose this to the Management and/or the Board if the Appointed Actuary considers that by doing so, the interests of policyholders may be jeopardized; or has lost confidence in the Board or Management of the Insurer.</p>		<p>bima au wakurugenzi wake wamekiuka Sheria ya bima au Sheria nyingine na ukiukwaji huo unapoteza maslahi ya wakata bima.</p> <p>6.2.5 Pale ambapo taarifa hiyo inawasilishwa moja kwa moja kwa Mamlaka, Mtathmini bima aliyeteuliwa hana wajibu wa kuwasilisha kwenye uongozi au Bodi iwapo mtathmini bima aliyeteuliwa anaona kwamba kwa kufanya hivyo maslahi ya wakata bima yatakua hatarini au amekosa imani na Bodi au Uongozi wa kampuni ya bima.</p>

SECTION SEVEN: PROHIBITED PRACTICES		SEHEMU YA SABA: UTEKELEZAJI	
7.1 Prohibition	<p>7.1.1 The Appointed Actuary shall not hold positions within or outside of the insurer that may create conflicts of interest or compromise his or her independence.</p> <p>7.1.2 Any person who contravenes the provision of these guidelines commits an offence and shall be subject to regulatory sanctions by the Commissioner of Insurance as per Insurance Act Cap 394.</p>	7.1 Makatizo	<p>7.1.1 Mtathmini bima aliyeteuliwa hatashika nafasi yoyote ya ndani au nje ya kampuni ya bima ambayo inaweza kusababisha migongano ya maslahi au kuathiri uhuru wake.</p> <p>7.1.2 Mtu yeyote anayekiuka matakwa ya miongozo hii anatenda kosa na atawajibishwa na Kamishna wa Bima kwa mujibu wa Sheria ya Bima Sura ya 394.</p>

SECTION EIGHT: REVIEW AND APPROVAL		SEHEMU YA NANE: MAPITIO NA IDHINI	
